# AMAZING TANZANIA

Toleo Na. 2 | JULAI 2025



- Asante Tanzania-Miss World Suchata
- TANZANIA YAJIPANGA KUANDAA MISS WORLD 2027

# YALIYOMO


1. Kutalii Tanzania kunatoa tiba ya afya ya akili-Profesa Hery- **UK. 1**
2. Mkuu wa Mabohora afanya"Royal Tour" Tanzania-**UK. 3**
3. Tanzania yaishukuru UNESCO kwa kulinda urithi wa dunia-**UK. 4**
4. Asante Tanzania-Miss World Suchata- **UK. 5**
5. Tanzania Yajipanga kwa "Miss World 2027"-**UK. 7**
6. Tanzania kuimarisha Hifadhi za Wanyamapori zinazovuka mipaka-**UK. 9**
7. TaFF YAJIVUNIA MIAKA MINNE YA RAIS DKT. SAMIA MADARAKANI-**UK. 11**
8. SONGEA: MJI WA MASHUJAA NA HAZINA YA URITHI WA HISTORIA YA MAJIMAJI-**UK. 12**
9. Sera Nzuri za Uwekezaji Zavutia Wawekezaji Sekta ya Utalii-**UK. 14**
10. TFS yapongezwa uhifadhi na utalii ikolojia Sao Hill- **UK. 16**
11. Tanzania, Uganda kushirikiana kuhifadhi maeneo ya Malikale-**UK.18**
12. Tanzania, India kuimarisha uwekezaji sekta ya utalii-**UK. 19**
13. Tanzania, Korea Kusini kuimarisha ushirikiano katika Sekta ya Utalii-**UK. 20**
14. Tanzania, Moroko, Ethiopia waendelea kuwa wababe utalii Afrika -**UK. 21**
15. Waziri Chana Ateta na Mkurugenzi wa UNESCO-**UK. 23**
16. Tanzania yaendelea kug'ara tuzo za "Best of the Best Awards" za TripAdvisor- **UK. 24**
17. Watu Zaidi ya Laki Sita Watembelea Banda la Maliasili Sabasaba 2025-**UK. 26**
18. Uwanja wa Gofu Ikoma: Zao Jipya la Utalii Serengeti-**UK.28**




# KUTALII TANZANIA KUNATOA TIBA YA AFYA YA AKILI-PROFESA HERY

## Na Mwandishi Wetu

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana amekutana na Profesa Chantal Henry mwandishi wa kitabu Tanzano-Therapie kinachozungumzia kwa undani jinsi mtu anaweza kupata tiba ya msongo wa mawazo kwa kutembelea maeneo ya hifadhi nchini Tanzania.



Prof. Henry ambaye ni Mkufunzi Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Paris East Creteil (UPEC) na mtaalamu wa afya ya akili nchini Ufaransa, ameeleza kuwa kitabu chake kimebeba matokeo ya utafiti alioufanya Tanzania kwa kushuhudia na kuchambua manufaa ya utalii katika hifadhi.

Anasema matokoe ya utafiti wake uliofanyika nchini Tanzania na ambao uko ndani ya kitabu hicho unaonesha kuwa mtu anavyoweza kupona changamoto za saikolojia ya akili na kuhuishwa kisaikolojia kwa kutembelea maeneo ya hifadhi na kuangalia wanyama na vitu vya asili.

"Nilitembelea hifadhi za Serengeti, Ngorongoro, hadi Gombe-Mahale nikiwa na familia yangu, kisha nikarudi kama mtafiti. Niligundua kuwa kutalii maeneo haya ya Tanzania kunatoa tiba kwa wagonjwa wa afya ya akili na hasa kwa watu wanaokabiliwa na msongo wa mawazo."

Prof. Henry anaongeza kuwa: "kutokana na uzoefu wangu na mahojiano na watalii mbalimbali, nimeanzisha kampeni barani Ulaya kuhimiza watu kutembelea Tanzania kwa ajili ya kujipatia tiba ya kisaikolojia kupitia vivutio vya kipekee."

Akizungumza baada ya mazungumzo hayo yaliyofanyika Paris, Ufaransa, Waziri Dk Pindi anasema kitabu hicho kitasaidia kuitangaza Tanzania na kuunga mkono juhudi za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia filamu za The Royal Tour na Amazing Tanzania.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt. Hassan Abbasi anasema watamshawishi Prof. Henry ili kitabu hicho kinatafsiriwa katika lugha mbalimbali zikiwemo Kiingereza na Kiswahili kwa lengo la kuwezesha kuwafikia watalii wengi zaidi duniani.






# MKUU WA MABOHORA AFANYA"ROYAL TOUR" TANZANIA

**Na Mwandishi Wetu**

Kiongozi Mkuu wa Madhehebu ya Kiislamu ya Bohora Duniani (Da'i al-Mutlaq), Syedna Mufaddal Saifuddin ametua nchini kwa ajili ya mapumziko ya kiutalii.

Saifuddin amepokelekwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Tabora na Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Dkt. John Mboya ambaye ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora na viongozi na waumini wa madhehebu ya Bohora nchini.

Kiongozi huyo wa kiroho mwenye wafuasi zaidi ya milioni 1 duniani na akisifika kwa mtazamo wake wa kutoa misaada ya kijamii, atakuwa kwenye faragha ya mapumziko kwenye vivutio vya kiutalii ukanda wa magharibi nchini.



# TANZANIA YAISHUKURU UNESCO KWA KULINDA URITHI WA DUNIA



**Na Mwandishi Wetu**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbasi, ameishukuru Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa mchango wake mkubwa katika kulinda maeneo ya Urithi wa Dunia barani Afrika, ikiwemo Tanzania.

Dkt. Abbasi alitoa shukrani hizo wakati kutoa salamu za Tanzania katika kikao maalum cha Kundi la Afrika (Africa Group) kilichofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 47 wa Kamati ya Urithi wa Dunia ya UNESCO uliofanyika Mjini Paris, Ufaransa.

Vikao vya Kundi la Afrika huandaliwa kwa lengo la kujadili masuala ya urithi wa dunia na kupanga mbinu za kushirikiana na mabara mengine wakati wa majadiliano ya pamoja ili kulinda maslahi ya Afrika.

Kikao hicho kilihudhuriwa pia na Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa, Mhe. Ali Mwadini, pamoja na wataalamu wa urithi kutoka Tanzania.

Dkt. Abbasi aliishukuru UNESCO kwa kuendelea kuzisaidia nchi za Afrika kulinda urithi wao.

Aidha, ripoti za hali ya uhifadhi kwa maeneo ya urithi wa dunia nchini Tanzania zilizowasilishwa mwaka huu zikiwemo Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Selous na Magofu ya Kilwa zimeidhinishwa na kupitishwa rasmi na vikao vya UNESCO.



# ASANTE TANZANIA



Miss World Suchata

## Na Mwandishi Wetu

MISS World 2025, Opal Suchata Chuangsri amefanya ziara ya siku kadhaa nchini Tanzania na kuelezea namna alivyovutiwa na mandhari ya kipekee, tamaduni na juhudi za kulinda uhifadhi na mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na vijavyo.

Akizungumza mara baada ya ziara yake, Suchata anasema:" nimekuwa na siku kadhaa ya kutembelea maeneo mbalimbali nchini Tanzania. Safari ilianzia Jiji la Dar es Salaam ambako tulipata fursa ya kujifunza tamaduni na kushuhudia ukarimu wa watu wake.

"Pia nimeenda Bahari Beach kwenye fukwe nzuri na nimejionea machweo ya jua kutokea Tanzania."



Suchata anaongeza kusema kuwa: “pia tulitembelea Hifadhi za Serengeti na Ngorongoro ambako tuliona uoto wa asili (nature) na ninathamini kwa dhati jinsi Tanzania inavyotunza uhifadhi wa asili kwa ajili ya kizazi chetu na vizazi vijavyo kuweza kushuhudia, kuona uhai unaotolewa na mazingira haya.”

“Ni muhimu sana kujifunza kutoka kwenu kwamba iwapo hatutaitunza sayari, nayo haitaweza kututunza sisi, hivyo ni muhimu dunia nzima ije kuona maeneo adimu nchini Tanzania na kuona jinsi mnavyoyatunza kwa upendo na uangalifu mkubwa.”



“Zanzibar pia ni miongoni mwa maeneo mazuri sana nchini Tanzania yenye watu wa wazuri, hivyo ziara yangu ilikuwa nzuri na yakuvutia sana. Asanteni sana Tanzania kwa kutukaribisha na kutupokea.”






# TANZANIA YAJIPANGA KUANDAA MIS WORLD 2027

Akiwa Zanzibar, mwanamaono, kiongozi thabiti na mwanamageuzi asiyechoka Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipata wasaa wa kuzungumza na uongozi wa kampuni ya Miss World Limited na kuridhia Tanzania kuwa mwenyeji wa mashindano hayo mwaka 2027.

Katika kikao hicho cha mazungumzo zilialikwa pia Sekta mbili za Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wizara ya Maliasili na Utalii.

"Hatua ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuridhia Tanzania kuanza maandalizi ya kuwa mwenyeji wa shindano hilo mwaka 2027 ni uamuzi ambao utafungua mafanikio lukuki kwa nchi ikiwemo katika uendelezaji wa vipaji, sanaa na utalii na zaidi kukuza chapa (brand) ya nchi katika dunia hii iliyosheheni ushindani," anasema Dkt. Hassan Abbasi Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili mara baada ya kikao hicho muhimu akifafanua namna utalii utakavyonufaika.








MISS WORLD AFRICA


MISS WORLD
MISS WORLD AFRICA



# TANZANIA KUIMARISHA HIFADHI ZA WANYAMAPORI ZINAZOVUKA MIPAKA

**Na Mwandishi Wetu**

Wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) katika kutekeleza mpango wa hifadhi na mifumo ikolojia inayovuka mipaka ya nchi mbili au zaidi.

Hatua hii inalenga kudhibiti ujangili, kulinda rasilimali na kukuza uchumi wa jamii kupitia utalii wa wanyamapori.

Akifungua kikao cha wataalamu wa ndani jijini Dodoma, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Kamishna wa Polisi (CP), Benedict Wakulyamba anasema mpango huo utafungua shoroba za wanyamapori na kuongeza kipato kwa wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi.

“Matumizi endelevu ya maliasili, ikiwemo uzalishaji wa asali na biashara ya kaboni, yataimarika kupitia utekelezaji wa mpango huu,” anasema CP Wakulyamba.





Anabainisha kuwa maeneo muhimu ya ushirikiano ni pamoja na usimamizi wa pamoja wa mifumo ikolojia, wanyamapori, misitu na vyanzo vya maji, sambamba na kuimarisha maendeleo ya kijamii kupitia fursa za utalii na biashara.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, Dkt. Fortunata Msoffe anasema kikao hicho kitalenga kuweka mpango wa kuanzishwa kwa Hifadhi ya Pamoja (TFCA) kati ya Tanzania na Zambia na kubaini fursa za ustawi wa jamii katika maeneo husika.

“Tanzania tayari inatekeleza ushirikiano na Msumbiji kupitia mfumo ikolojia wa Selous–Niassa tangu mwaka 2007, na mpango huu mpya utapanua wigo wa usimamizi wa rasilimali zinazovuka mipaka kwa faida za kiuchumi na kiikolojia,” anasema Dkt. Msoffe.

Mpango huo ni unatekeleza maazimio ya mkutano wa wakuu wa nchi za SADC uliofanyika Harare, Zimbabwe, Mei 2025 ukilenga kuimarisha hifadhi zinazovuka mipaka kwa manufaa ya kiuchumi na kiikolojia.



# TaFF YAJIVUNIA MIAKA MINNE YA RAIS DKT. SAMIA MADARAKANI

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) umetoa zaidi ya Sh bilioni 20 katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kusaidia usimamizi, uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki nchini.

Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) Dkt. Tuli Salum Msuya amesema fedha hizo zimetolewa kama ruzuku kwa wadau mbalimbali na taasisi ili kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na misitu na nyuki, kwa manufaa ya jamii na taifa kwa ujumla.

Akizungumza hivi karibuni mkoani Tabora wakati wa ukaguzi wa miradi iliyofadhiliwa na TaFF kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Dkt. Mbwambo alisema fedha hizo zimetokana na uongozi bora wa Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na jitihada za ukusanyaji wa maduhuli ya misitu zinazofanywa na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS).

“Fedha hizo zimetumika kuwezesha vikundi vya uhifadhi na ufugaji nyuki, kufanya tafiti, kufadhili masomo kwa wanafunzi na kujenga miundombinu katika vyuo vya misitu na ufugaji nyuki vilivyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ikiwemo Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora, Chuo cha Misitu Olmotonyi na Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi,” alisema Dkt. Msuya.

Naye Mkuu wa Miradi na Mpango Dkt. John Richard amesema Mfuko huo pia umefadhili tafiti za mchango wa sekta ya misitu na nyuki katika Pato la Taifa, tafiti za magonjwa na uzalishaji kwenye mashamba ya miti, pamoja na utafiti wa aina mbalimbali za mizinga na asali, ili kuboresha ubora na thamani ya mazao hayo kwa soko la ndani na nje ya nchi.



Kwa upande wake, Mkuu wa Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora (BTI), Semu Daudi anasema miradi inayofadhiliwa na TaFF imewezesha ujenzi wa jengo la mihadhara, karakana na kituo cha kuchakata asali jambo litakaloboreshwa mazingira ya ufundishaji na na ujifunzaji hivyo kuzalisha wataalamu wenye ujuzi na watakaosaidia kukuza mnyororo wa thamani wa mazao ya nyuki. nchini.

“Mfuko wa Misitu Tanzania umetupatia zaidi ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa jengo kubwa la mihadhara ambalo ujenzi wake umefikia zaidi ya asilimia 70, na pia umetoa ufadhili kwa wanafunzi wa ngazi ya Shahada na Astashahada,” anasema Bw. Daudi






# SONGEA: MJI WA MASHUJAA NA HAZINA YA URITHI WA HISTORIA YA MAJIMAJI

**Na Mwandishi Wetu**

Mji wa Songea ni eneo lililobeba kumbukumbu kuu za mashujaa waliopigana kwa ujasiri dhidi ya ukoloni wa Kijerumani katika Vita ya Majimaji ya mwaka 1905 hadi 1907.

Historia inatuambia kwamba zaidi ya mashujaa 67 walinyongwa katika Mji wa Songea mwaka 1906 kwa kosa moja tu kupinga kwa ujasiri utawala wa Kijerumani. Kati yao, mashujaa 66 walizikwa pamoja katika kaburi moja, ishara ya umoja na ujasiri usioyumba.

Nduna Songea Mbano, mmoja wa viongozi waliokuwa na ushawishi mkubwa, alinyongwa peke yake na kuzikwa katika kaburi lake, ambalo hadi leo linaheshimiwa ndani ya Makumbusho ya Majimaji mjini Songea.

Makumbusho hayo yaliyofunguliwa rasmi mwaka 1980 chini ya usimamizi wa Hayati Dkt. Lawrence Gama, yameendelea kuwa kitovu cha kumbukumbu ya harakati za ukombozi.

Mwaka 2010, yalikabidhiwa rasmi kwa Shirika la Makumbusho ya Taifa na kupandishwa hadhi kuwa Makumbusho ya Taifa ya Majimaji chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii hatua iliyoongeza mvuto wa kiutalii na kuimarisha hifadhi ya urithi wa kipekee.

Makumbusho ya Taifa ya Majimaji ni ya aina yake nchini Tanzania yakihifadhi silaha halisi za vita ya Majimaji, nguo, picha na ramani halisi za mapigano.





wizarayamaliasilinautalii

Takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya wageni 10,000 hutembelea makumbusho hayo kila mwaka, wengi wao wakiwa ni wanafunzi, watafiti na watalii wa kimataifa wanaotaka kujifunza historia halisi ya mapambano ya wazawa wa Afrika dhidi ya ukoloni.

Lakini Songea haikujikita tu katika Vita ya Majimaji. Mkoa wa Ruvuma ulitoa mashujaa 270 waliopigana katika Vita Kuu ya Pili ya Dunia kati ya 1939 hadi 1945, na miongoni mwao mashujaa hao watatu walikuwa wanawake ambao ni nadra katika simulizi nyingi za vita vya dunia.

Aidha mbali na Makumbusho ya Taifa ya Majimaji, sanamu za wapiganaji maarufu wa Majimajii za Mpambalyoto Soko bin Msarawani, Nduna Songea Mbano bin Luwafu, Zimamoto Gama bin Fusi, na Nduna Usangira majina yanayosikika kama mashairi ya uhuru.

Kwa wenye shauku ya kutafakari historia kwa macho, makaburi ya mashujaa 66 ni sehemu ya kivutio ambacho hutetemesha moyo wa mzalendo yeyote. Hapo ndipo ilipo roho ya Songea Mbano.





# SERA NZURI ZA UWEKEZAJI ZAVUTIA WAWEKEZAJI SEKTA YA UTALII

**Na Mwandishi Wetu**

Sera nzuri ya uwekezaji, mazingira wezeshi pamoja na ushirikiano wa muda mrefu na Serikali ya Tanzania yamekuwa kichocheo kikubwa cha kuvutia wawekezaji hususan mtandao wa Hoteli za Neptune kuendelea kuwekeza zaidi katika sekta ya utalii nchini Tanzania.



Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa Mtandao wa Kampuni ya Hoteli za Neptune, Amin Mohamed Merali hivi karibuni alipotembelea ujenzi wa hoteli mpya na ya kifahari ya Neptune inayojengwa katika vilima vya Soroi ndani ya Hifadhi ya Serengeti

Amesema mahusiano bora na ya muda mrefu na Serikali ya Tanzania pamoja na ziara zake zangu za mara kwa mara nchini na kuona maendeleo yaliyopatikana pamoja na mazingira bora ya uwekezaji ni baadhi ya vitu vilivyochochea dhamira yangu ya kuanza kujenga hoteli nyingine katika hifadhi na katika vivutio vingine vya utalii.

“Maono yangu ni zaidi ya biashara, ni juu ya kuwezesha jamii na Taifa kwa ujumla, ni kutengeneza miradi itakayokua chanzo cha Ajira zitakazowezesha kustawisha jamii za watanzania huku tukiendelea kukuza Uchumi wa nchi kupitia uwekezaji wa kimkakati kwenye Sekta ya Utalii”

Ameongeza kuwa ujenzi wa hoteli hii inakua hoteli ya tatu ya mtandao wa Hoteli za Neptune kwa Tanzania baada ya ile ya Ngorongoro na Zanzibar na ujenzi utagharimu Dola za Marekani milioni 10 na itakuwa katika muundo wa ‘Luxury Tent’ ikiwa na nyumba 20 za kulala wageni.

Naye Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa Neptune Hotel, Bw. Clemens Faber, akieleza hatua za ujenzi wa hoteli hiyo amesema" Itakapokamilika na kufunguliwa rasmi mwezi Novemba 2025, itakuwa na uwezo wa kuhudumia kati ya watu 20 hadi 80, ikiwa tayari kwa msimu wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, Wageni watakuwa na nafasi ya kushuhudia wanyama kutoka ndani ya vyumba vyao, kutokana na eneo la juu ilipojengwa hoteli hiyo.



“Tumetengeneza mnara wenye darubini utakaowawezesha kuona eneo kubwa la Serengeti na Wanyama waliopo kutokea hotelini,"amesema.

Kwa mujibu wa Faber, hoteli hiyo inajengwa kwa kuzingatia uzalendo, kwani zaidi ya wafanyakazi 200 wanaoshiriki katika mradi huo ni Watanzania na vifaa vyote vya ujenzi vinapatikana nchini.

Kwa upande wake, Meneja Mkuu wa Neptune Serengeti, Rakesh Prasad, amesema mbali na kuongeza fursa za malazi kwa watalii, hoteli hiyo mpya inachangia kutoa ajira kwa Watanzania zaidi ya 90 itakapofunguliwa rasmi.

Serengeti, ikiwa ni hifadhi ya tatu kwa ukubwa nchini baada ya Nyerere na Ruaha, hupokea zaidi ya watalii 450,000 kila mwaka na imekuwa ikishinda tuzo nyingi za kimataifa, hali inayoiweka kileleni mwa vivutio vya utalii Afrika Mashariki.



# TFS YAPONGEZWA UHIFADHI NA UTALII IKOLOJIA SAO HILL

**Na Mwandishi Wetu**

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umepongezwa kwa juhudi kubwa zinazofanyika katika uhifadhi wa misitu, ukuzaji wa utalii ikolojia, ufugaji nyuki na ukusanyaji wa mapato ya serikali kupitia Shamba la Miti la Sao Hill mkoani Iringa.



Pongezi hizo zimetolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Mipango katika Wizara ya Maliasili na Utalii, Bw. Abdallah Mvungi wakati wa ziara ya viongozi wa wizara hiyo waliotembelea Shamba hilo ili kujionea shughuli za uhifadhi na maendeleo ya utalii unaoibukia katika misitu ya asili.

Anasema kutokana na uwekezaji wa Serikali, TFS imeendelea kuekeleza majukumu yake kwa ufanisi, hususan katika usimamizi wa misitu ya kupandwa na ile ya asili Shamba la Miti Sao Hill.

"Tuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuiwezesha TFS, kwa kweli TFS imefanyakazi kubwa ya uhifadhi wa misitu huku ikibuni njia mpya za kukuza utalii ikolojia unaotegemea mazingira ya asili kama vile maporomoko ya maji, miinuko ya kuvutia na wanyamapori waliopo kwenye misitu ya asili."

Alisema pia kwa kimarisha utalii wa michezo kama mbio za marathoni, baiskeli na magari, hatua inayosaidia kuongeza mapato kupitia vyanzo vipya.



“Nichukue fursa hii kutoa wito kwa wananchi na wadau wa utalii kutembelea maeneo hayo ili kuchangia maendeleo ya sekta hiyo.



Bw. Mvungi pia aliipongeza TFS kwa mkakati wa kukabiliana na majanga ya moto kwa kutoa elimu kwa jamii zinazozunguka shamba na kuzijengea uelewa wa namna ya kudhibiti uchomaji moto holela.

Kwa upande wa Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti Sao Hill, PCO Tebby Yoramu alisema mafanikio hayo yanatokana na ushirikiano mzuri kati ya shamba na jamii jirani hasa kupitia utoaji wa elimu ya uhifadhi na usambazaji wa miche ya miti kwa ajili ya kuhifadhi mazingira.






# TANZANIA, UGANDA KUSHIRIKIANA KUHIFADHI MAENEO YA MALIKALE

**Na Mwandishi Wetu**

Tanzania na Uganda zimekubaliana kuendelea kushirikiana katika uhifadhi wa maeneo ya malikale yaliyopo katika nchi hizo mbili.

Makubaliano yamefikiwa wakati wa katika cha pamoja kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii wa Tanzania, Dkt. Hassan Abbasi, na mwenzake wa Uganda, Katibu Mkuu wa Utalii, Wanyamapori na Malikale, Mama Doreen Katusiime.

Kikao hicho, kilichoshirikisha pia wataalam wa pande zote mbili, kimefanyika pembezoni mwa Mkutano wa 47 wa Kamati ya Urithi wa Dunia ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kilichofanyika jijini Paris, Ufaransa.

Tanzania na Uganda zina maeneo yenye urithi wa kihistoria yanayofanana, yakiwemo michoro ya kale ya miamba katika eneo linalozunguka ukanda wa Ziwa Viktoria.

Ushirikiano huu unalenga kuboresha uhifadhi na kuendeleza utalii wa urithi wa dunia katika ukanda huo.






# TANZANIA, INDIA KUIMARISHA UWEKEZAJI SEKTA YA UTALII



Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana, amefanya mazungumzo na Balozi wa India nchini Tanzania, Bw. Bishwadip Dey kuhusu kuimarisha ushirikiano kati ya mataifa hayo mawili katika sekta ya utalii.

Mazungumzo hayo yamefanyika katika Chuo cha Taifa cha Utalii, jijini Dar es Salaam, yakilenga kuvutia wawekezaji zaidi kutoka India kuja kuwekeza nchini Tanzania.

Waziri Chana anasema serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji, huku ikihamasisha fursa mbalimbali zilizopo katika sekta ya utalii.

Kwa upande wake, Bw. Dey ameahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kukuza uwekezaji na kubadilishana uzoefu unaolenga kuimarisha sekta hiyo.



# TANZANIA, KOREA KUSINI KUIMARISHA USHIRIKIANO KATIKA SEKTA YA UTALII

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana, amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Korea Kusini nchini Tanzania, Mhe. Eunju Ahn, katika kikao kilichofanyika jijini Dar es Salaam.

Mazungumzo hayo yalilenga kuimarisha ushirikiano baina ya Tanzania na Korea Kusini kupitia sekta ya utalii, ikiwemo kubadilishana uzoefu na kuendeleza miradi ya pamoja itakayosaidia kuvutia watalii zaidi kutoka mataifa hayo mawili.

Katika mazungumzo hayo walijadili mpango wa kuboresha Chuo cha Taifa cha Utalii katika nyanja mbalimbali, ili kuongeza ubora wa mafunzo na kuandaa wataalamu wenye ujuzi wa kimataifa katika sekta ya utalii.

Dkt. Chana amesema lazima tuhakikishe tunakua na Utalii endelevu utakaomnufaisha kila mmoja wetu , licha ya mafanikio yaliyopatikana kwa upande wa wageni na mapato, juhudi zaidi zinahitajika ili kuweza kuongezeka maradufu kwa idadi na wageni na mapato yetu kwa ujumla na kuhakikisha pia jamii inanufaika.





# TANZANIA, MOROKO, ETHIOPIA WAENDELEA KUWA WABABE UTALII AFRIKA

**Na Mwandishi Wetu**

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii (UN Tourism Q1, 2025) ikisheheni takwimu za utalii duniani mpaka Mei mwaka huu, imeonesha kuwa Tanzania imeendelea kufanya vyema kiutalii Afrika na Duniani kwa takwimu za robo ya kwanza ya mwaka huu katika vyote;

Ongezeko la watalii na mapato ikilinganishwa na mwaka 2019 kabla ya Uviko. Ongezeko la Watalii kwa Dunia na Afrika Tanzania imeingia tatu bora ya nchi za Afrika zinazoongoza kwa ongezeko la watalii wengi ikilinganishwa na mwaka 2019 kwa kupata ongezeko la watalii kwa asilimia 50 ikitanguliwa na Moroko (asilimia 60) na Ethiopia (asilimia 52).

Kwa matokeo hayo Tanzania ni miongoni mwa nchi 20 bora duniani kwa ongezeko kubwa la watalii inapolinganishwa na mwaka 2019 ikitanguliwa na mataifa kama Brazil, Albania, Qatar na Saudia.

Ongezeko la Mapato Kidunia na Afrika Katika kipengele hiki, kwa Afrika, inaonesha ripoti hiyo, Tanzania imeongoza kwa kuongeza mchango au mapato ya sekta hiyo kwa asilimia 66 ikilinganishwa na mwaka 2019 na hivyo kuwa ya kwanza Afrika (ikifuatiwa na Tunisia 62% na Moroko 49%).



Kwa takwimu hizo Tanzania ni nchi ya 12 duniani ikiwa orodha moja na mataifa kama Norway, Brazil, Qatar, Saudia, Moldova n.k. Nini Kimetokea Tanzania? Alipoulizwa kuhusu mafanikio hayo Katibu Mkuu wa Utalii na Mwenyekiti wa Kamati ya Rais ya Kuitangaza Tanzania, Dkt. Hassani Abbasi anasema akiwa Paris Ufaransa kikazi: "Ni mikakati. Tusingepata mafanikio haya kwa kukaa ofisini kufanya michakato miingi na kuchambua nyaraka."

"Mhe Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoka ofisini akaenda "field" akafanya filamu za Royal Tour na Amazing Tanzania; viongozi wetu wa Wizara, mabalozi wetu kote duniani, taasisi zetu na wadau wametoka kwenda kuitangaza nchi ama ana kwa ana au kushiriki maonesho makubwa.


Mbegu hizo ndio zimeleta mavuno haya. "Kwetu sisi maono ya kwenda mbele ni kuwaza mikakati zaidi ikiwemo kupitia kujitangaza kwenye ligi kubwa duniani. Ukiangalia ile ripoti utaona Qatar na Saudia wako juu ni matokeo ya mikakati pia ya vitu kama michezo na matamasha yanayofuatiliwa na nchi nyingi," alisema Dkt. Abbasi.


Alipoulizwa matokeo hayo yanasadifu vipi uhalisia? Anajibu: "Kwanza nchi yetu imefurika watalii kila kona hapa tunavyoongea, lakini ukiangalia takwimu zetu zinaendana na hizo za UN Tourism. Hakuna palipopungua.



Taarifa ya juzi ya BoT inaonesha sekta hii imeleta Dola Bilioni 3.92 kwenye uchumi ikiwa namba moja kuleta fedha za kigeni. Makusanyo ya maduhuli kwa taasisi zote kubwa za utalii Tanapa, TFS, Tawa na Mamlaka ya Ngorongoro yamefikia viwango ambavyo havijapata kutokea tangu zianzishwe.

"Mfano katika masoko makubwa tumejitangaza sana utaona Marekani ongezeko la watalii kuja ni 41% China na India leo watalii kutoka China wameongezeka kwa asilimia 108 na kutoka India ni asilimia 75. Kona zote tunaona watalii na mapato vikiongezeka. Narudia tena na shika sana neno hili MIKAKATI."






# WAZIRI CHANA ATETA NA MKURUGENZI WA UNESCO

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana Julai 10, 2025 amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Msaidizi wa UNESCO anayeshugulikia masuala ya Utamaduni, Bw. Ernesto Ottone, pembezoni mwa Mkutano wa 47 wa Kamati ya Urithi wa Dunia unaoendelea mjini Paris, Ufaransa.

Kupitia kikao hicho, viongozi hao wameazimia kuimarisha ushirikiano kati ya UNESCO na Tanzania katika uhifadhi wa Maeneo ya Urithi wa Dunia yaliyopo nchini Tanzania.

Kadhalika, Mkurugenzi huyo ameahidi kuimarisha ushirikiano katika uendelezaji wa shughuli za kiutamaduni nchini Tanzania na kukuza uhifadhi wa vivutio vyake vya kipekee.

Kikao hicho kimehudhuriwa pia na Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa Mhe. Ali J. Mwadini, pamoja na wataalam wengine kutoka Tanzania.






04.

**Serengeti Balloon Safari and authentic bush breakfast**

Seronera, Tanzania

## TANZANIA YAENDELEA KUG'ARA TUZO ZA "BEST OF THE BEST AWARDS" ZA TRIPADVISOR

**Na Mwandishi Wetu**

MATOKEO ya utafiti kupitia maoni ya watalii uliofanywa na mtandano maarufu duniani kwa biashara ya utalii kidigiti wa TripAdvisor, Tanzania imechomoza tena katika tuzo baada ya vivutio vyeka kung'ara kwenye tuzo za Travelers' Choice: Best of the Best Awards.


Tanzania imeng'ara katika tuzo hizo kutokana na kura zilizopigwa na mamilioni ya watalii duniani wanaliopiga kura kwa maeneo waliyoyatembelea na kubaki mioyoni mwao kutokana na uzoefu wa kipekee walioupata.

Kampuni ya TripAdvisor yenye makao yake makuu Needham, Massachusetts, Marekani, huhudumia takribani maombi milioni 350 kwa mwezi na ina wateja waliosajiliwa takribani milioni 900, ikitoa huduma za malazi, usafiri na malipo ya maeneo ya kutembelea.

Tuzo za "Travelers Choice: Best of the Best Awards" huwapa fursa mamilioni ya wateja wa kampuni hiyo duniani kupiga kura kwa kutaja maeneo waliyotembelea na yakabaki daima mioyoni mwao.

Katika kipengele cha "Bucketlist Experiences", kinachoangalia huduma na uzoefu wa kipekee kwa watalii, safari ya baluni katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imeshika nafasi ya nne duniani na kuvizidi baadhi ya vivutio maarufu duniani kama Scuba diving ya Honolulu, Hawaii (5), Safari ya jioni ya Jangwani, Dubai (6) na Hanoi, Vietnam Motorbike Tour (7).

Aidha, Ngorongoro na Tarangire pia zimeorodheshwa, zikishika nafasi ya 6 na 10 mtawalia katika orodha ya vivutio 25 bora barani Afrika, kwenye kipengele cha "Top Attractions" kinachohusisha maeneo yanayovutia watalii zaidi.




Pia safari ya siku tano inayounganisha vivutio vya Ngorongoro, Serengeti, Tarangire na Manyara imetajwa kuwa kivutio bora namba nane barani Afrika, ikionyesha hadhi ya Tanzania kama kinara katika sekta ya utalii duniani.






# WATU ZAIDI YA LAKI 6 WATEMBELEA BANDA LA MALIASILI SABASABA 2025

## Na Mwandishi Wetu

Banda la Wizara ya Maliasili na Utalii kwenye Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba 2025) limevutia watu 660,000 kutokana na mvuto wa huduma na vivutio vinavyotolewa na idara na taasisi zake.




Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Afisa Masoko Mwandamizi, Bi. Flaviana Moshi anasema mwitikio huo mkubwa ni matokeo ya maandalizi mazuri yaliyofanywa na wizara kupitia Bodi ya Utalii.

“Wageni waliotembelea banda hilo wamepatia mbalimbali ikiwemo kufanya utalii wa wanyamapori hai na kupata bidhaa za misitu na nyuki, pamoja na huduma za utafiti na malikale.”

Kwa upande wake, Mzee Rashidi Jumanne, mkazi wa Mbagala alieleza kufurahishwa na mpangilio wa banda hilo na ameridhishwa huduma ya nyama ya wanyamapori na vyakula mbalimbali.

“Nimefundishwa kwenye meza ya Chuo cha Utalii namna ya kuandaa meza ya chakula kwa wageni, nimekula nyama choma ya swala, na nimeondoka na miche yangu ya miembe ambayo naenda kupanda nyumbani.”







# UWANJA WA GOFU IKOMA: ZAO JIPYA LA UTALII SERENGETI

**Na Mwandishi Wetu**

Wakati wakisubiri ndege yao katika eneo la Fort Ikoma, watalii wawili, Richard Thelene na Corinne Thelene ambao ni mtu na mkewe kutoka nchini Ufaransa wanatembea kuelekea eneo ambalo linaandaliwa kuwa uwanja wa mchezo wa kimataifa wa Gofu.

Richard ni mchezaji wa Gofu na pia anadhamini klabu ya mchezo huo, nchini ufaransa. Yeye na mkewe baada ya kufanya utalii katika mbuga ya Serengeti, wamejikuta eneo la uwanja wa Fort Ikoma.

Watalii wao wamefurahishwa na ongezeko la kivutio hicho katika hifadhi ya Serengeti na kwamba mara utakapokamilika watakuwa miongoni mwa wachezaji wa kimataifa kuja kucheza Serengeti.

Katika harakati za kuongeza idadi ya watalii na kipata cha taifa, Bodi ya Wadhamini ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) imeelekeza uongozi wa shirika kutekeleza mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Gofu.





wizarayamaliasilinautalii

Mradi unatekelezwa katika eneo la ekari 450, utakuwa miongoni mwa viwanja virefu zaidi vya gofu duniani, ukiwa na kilomita 7.065, ambapo mchezaji atatembea kilomita 3.528 kwa mashimo ya ndani na kilomita 3.537 kwa mashimo ya nje.

Mmoja wa wasimamizi wa mradi, Bryceson Nyenza kutoka kambi ya Lugalo, Dar-es-salaam anasema kuwa uwanja wa Golf Serengeti, kwa upande wa eneo la kuchezea umekamilika kwa asilimia 85.

"Tunataraji kuwa michezo inaweza kuanzania kufanyika hapa mwezi Januari 2026," anasema Nyanza.

Uwanja huo kwa ajili ya mchezo huo wa 'Gofu,' unaotajwa kupendwa na watu matajiri, upo pembezoni mwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti eneo la Fort Ikoma kuelekea Mugumu mkoani Mara.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Tanapa Investment Company Limited (TIL) Richard Matolo, ambaye ndiye mhandisi wa mradi alisema kuwa gharama za ujenzi ni Shilingi bilioni 9.5.



Viwanja 15 kati ya 18 vimekamilika sambamba na utandazaji wa mabomba ya umwagiliaji chini ya ardhi.

Watalii watavutiwa zaidi kucheza kati uwanja wa Serengeti kwa sababu ya uwepo wa wanyamapori kama swala na pundamilia pembezoni mwa eneo ambao huongeza mvuto wa tukio zima.



# ONGEZEKO LA UTALII TANZANIA (2025)

## Jumla ya watalii walioingia nchini

(jan-2025 - Mei 2025)

**794,102**

Rekodi mpya ya miaka 10 iliyopita

## Ulinganisho wa watalii


(Mei-2024 Vs Mei 2025)

**28,000**

**+4%**

Ongezeko ikilinganishwa na 2024

## Idadi ya watalii (Januari - Mei)




## Watalii kwa Mwaka 2024

**2,141,895**

**178,000**

Wastani wa watalii kwa mwezi


## Watalii kwa Mwaka 2021

**788,933**

**+132.1%**

Ongezeko 2024 ikilinganishwa na 2021

## Tanzania Imeongoza Afrika kwa Ukuaji wa Utalii (2024)




## Mapato ya utalii wa kimataifa

**2021: Sh3.4 trilioni**

**2024: Sh10 trilioni**

**+200%**

Ongezeko la mapato 2024 ikilinganishwa na 2021

## Sababu Mafanikio ya utalii nchini

- **Filamu: The Royal Tour na Amazing Tanzania**
- **Digital marketing & ushirikiano na sekta binafsi**
- **Kampeni: "Talii Kijanja" & "Likizo Time"**
- **Miundombinu bora: Barabara, viwanja vya ndege, ATCL**
- **Utangazaji kupitia watu mashuhuri**
- **Mikutano ya kimataifa: (nishati & utalii wa vyakula)**

**MwananchiData** Imeandaliwa na Daniel Masubi

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, wadau


## WATALII WA KIMATAIFA WALIYOINGIA NCHINI

**Idadi ya watalii walioingia nchini kwa mwezi Jan-Jun, 2024-2025**


| MWENZI | 2024 | 2025 | ONGEZEKO | |
|---|---|---|---|---|
| | | | IDADI | ASILIMIA |
| JAN | 180,422 | 195,946 | 15,524 | 8.6 |
| FEB | 184,092 | 190,313 | 6,221 | 3.4 |
| MAR | 155,810 | 140,597 | - 15,213 | -9.8 |
| APRIL | 116,280 | 130,340 | 14,060 | 12.1 |
| MEI | 129,492 | 137,365 | 7,873 | 6.1 |
| JUN | 179,264 | 202,226 | 22,962 | 12.8 |
| JAN-JUN | 945,360 | 996,787 | 51,427 | 5.4 |

# IDADI YA WATALII WA KIMATAIFA KWA MADHUMUNI YA SAFARI JAN-JUN 2024-2025

**2a: Idadi ya watalii wa kimataifa**




**2b: Ongezeko la watalii kwa madhumuni ya safari (%)**




**2c: Mgawanyiko wa watalii kwa madhumuni ya safari (%)**

